**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN,**
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**KWENYE SHEREHE ZA BARAZA**
**LA EID EL-FITR KITAIFA**
**DAR ES SALAAM, TAREHE 14 MEI, 2021**

*Mheshimiwa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania,*
*Sheikh Abubakar Zubeir bin Ally Mbwana;*

*Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu*
*wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu*
*wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano*
*wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Prof. Ibrahim Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;*

*Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Ulamaa;*

*Wajumbe wa Bodi ya Udhamini ya BAKWATA;*

*Sheikh Khamis Hamisi Mataka, Mwenyekiti*
*wa Halmashauri Kuu ya BAKWATA;*

*Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge mliopo;*

*Mheshimiwa Abubakar Mussa Kunenge,*
*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Ustadh Nuhu Jabir Mruma, Katibu Mkuu wa BAKWATA;*

*Alhaj Abubakar Khalid Hajj, Mshauri Mkuu wa Mufti;*

*Hajjat Shamim Khan, Mwenyekiti wa JUWAKITA Taifa;*

*Sheikh Alhad Mussa Salum, Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam*
*pamoja na Masheikh wengine wa Mikoa mliopo;*

*Waheshimiwa Viongozi mbalimbali wa BAKWATA ngazi zote;*

*Waheshimiwa Masheikh, Maimamu na Makhalifa;*

*Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa;*

*Waheshimiwa Viongozi mbalimbali wa Dini mliopo;*

*Viongozi wengine wa Serikali mliopo;*

*Waheshimiwa Wageni wote Waalikwa;*

*Ndugu wana-Habari, Kinababa na Kinamama:*

**Assalaam Eleykum Warahmattullah Taallah wa -Barakatuh!**

**Eid-Mubarak!**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Napenda nianze kwa kuungana na wote walionitangulia kuzungumza katika kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutuweka hai na kutuwezesha kuiona siku ya leo. Wapo wenzetu wengi tu ambao walitamani kuiona siku ya leo lakini hawakuweza; na wapo ambao wameiona lakini kwa sasa wapo *ma*-Hospitalini au majumbani wamelala wakisumbuliwa na maradhi mbalimbali. Mwenyezi Mungu awape afya. Insha Allah. Hivyo basi, sisi tuliobahatika kuiona siku ya leo na kuweza kukusanyika hapa, hatuna budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kutupa afya njema.

Napenda pia nimshukuru sana Mheshimiwa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir Ally pamoja na Uongozi mzima wa BAKWATA, kwa kunialika kuja kujumuika nanyi kwenye shughuli hii. Leo ni mara yangu ya kwanza kuwa Mgeni Rasmi kwenye Baraza la Eid. Hivyo basi, nawashukuru sana kwa heshima hii kubwa mliyonipa, japokuwa imekuja na changamoto yake. Nimejiuliza nitaongea nini mbele ya masheikh. Lakini, nitajitahidi.

***Mheshimiwa Mufti na Ndugu Waislamu;***

Kama alivyosema Katibu Mkuu wa BAKWATA kwenye Salamu zake za Eid El Fitri, mwaka huu, Taifa letu limepita katika mtihani mgumu wa kuondokewa na aliyekuwa Kiongozi wetu, Hayati Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Hivyo basi, kabla sijaendelea zaidi, napenda kutumia fursa hii kurudia tena kuwashukuru Masheikh pamoja na Viongozi wote wa Dini

nchini kwa dua na sala zenu zilizotuwezesha kuvuka salama kwenye mtihani huo mkubwa uliotukumba.

Binafsi, nataka nirudie kuwashukuru viongozi wa dini nchini kwa kuwa nami bega kwa bega tangu niapishwe kuwa Rais wa nchi yetu. Nimefurahi kwenye Salamu zenu za Eid, BAKWATA mmeahidi kuendelea kunipa ushirikiano mimi binafsi pamoja na Serikali. Ahsanteni sana.

***Mheshimiwa Mufti;***
***Waheshimiwa Masheikh na Ndugu Waislamu;***

Eid El Fitr ni Sikukuu muhimu sana kwa waumini wa dini ya Kiislamu. Ni siku ambayo Waislamu duniani kote wanatoa shukran kwa Mwenyezi Mungu kwa kumaliza Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenyewe amesema kwenye Qur-an, nanukuu *"…..**Na mtimize hiyo hesabu (yaani Funga ya mwezi***

***Mtukufu wa Ramadhani) na Mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kuwa amekuongoeni ili mpate kushukuru"***, mwisho wa kunukuu (**Korani 2 - 185**).

Hivyo basi, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba yangu binafsi, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Waislamu wote nchini kwa kumaliza salama Funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani; nguzo ya nne ya Uislamu. Hongereni sana. Ni imani yangu kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu amezikubali funga zetu na kutusamehe madhambi yetu yote. Na katika hilo, napenda niungane na wote walionitangulia kuzungumza katika kuwasihi ndugu zangu Waislamu kuwa, ucha Mungu tuliouonesha kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani tuuendeleze. Usiishie jana baada ya kuandama kwa mwezi.

Tuendelee kutenda matendo mema yenye kumpendeza Mwenyezi Mungu; na tujiepushe kutenda matendo mabaya

yenye kumchukiza. Miongoni mwa matendo mema ni kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu. Na hapa napenda kuwasihi sana watumishi wa Serikali pamoja na sekta binafsi kuhakikisha wanafanya kazi na kupata kipato halali. Wajiepushe na vitendo vya wizi, rushwa, ubadhirifu na urasimu. Kwa upande wa wafanyabiashara, nawahimiza kulipa kodi stahiki kwa Serikali. Si haki wala uungwana kwa mfanyabiashara kukwepa kulipa kodi. Kufanya hivyo, kutaifanya Serikali ishindwe kutoa huduma muhimu kwa wananchi. Hospitali zetu zitakosa madawa na kusababisha vifo, watumishi watakosa mishahara na haki zao stahiki; na wanafunzi watakosa elimu bora.

Hivyo basi, napenda kurudia kusisitiza umuhimu wa kila mmoja wetu kuendelea kuishi matendo mema tuliyoyaishi wakati wa Funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Na binafsi naamini, endapo tutafanya hivyo, baraka na neema za

Mwenyezi Mungu Muumba tulizozipata kipindi cha Mfungo zitabaki nasi daima.

Nitumie fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza waumini wa dini nyingine, ambao kwa namna moja ama nyingine, walishirikiana na Waislam katika kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani: Iwe kwa kufunga; au kwa kujizuia kufanya baadhi ya mambo ya kuwakwaza waliofunga; ama kwa kushirikiana wakati wa futari.

Na hii ndiyo sifa na uzuri wa Tanzania. Pamoja na tofauti zetu za dini, kabila, rangi ama itikadi; tumekuwa tukishirikiana kwenye masuala mbalimbali. Nimefurahi kuona kwenye Baraza hili la Iddi wapo pia viongozi wa dini nyingine. Hatuna budi kuendeleza utamaduni huu ambao tumerithishwa na Waasisi wa Taifa letu.

***Mheshimiwa Mufti,***
***Ndugu Waislamu na Wananchi kwa ujumla;***

Hivi punde tumetoka kusikiliza Salamu za Iddi ambazo zimesomwa na katibu Mkuu wa BAKWATA. Tumezisikia pia nasaha kutoka kwa Mufti. Kwa ujumla, wote wamegusia mambo mengi muhimu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Taifa letu. Mojawapo ni kuhusu umuhimu wa kutunza amani, ambapo Katibu Mkuu wa BAKWATA alinikuu maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyomo kwenye Quran Tukufu; ambayo naamini yamo pia kwenye Biblia. Nitumie fursa hii, kuwahakikishia ndugu zangu Waislamu pamoja na Watanzania wote kwa ujumla, kwamba, Serikali itakuwa imara katika kuhakikisha amani na usalama vinaendelea kudumu. Nawasihi wananchi kutoa ushirikiano kwa Serikali; kama mnavyofahamu, jukumu la kulinda amani ni letu sote.

Sambamba na kutunza amani, Salamu zimegusia suala la kukuza uchumi. Naishukuru sana BAKWATA kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza uchumi, ikiwemo hatua tunazochukua za kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara. Nimefurahi pia kusikia kwamba BAKWATA mmejipanga kuanzisha miradi kwa ajili ya kukuza uwezo wa kiuchumi wa Taasisi na mtu mmoja mmoja. Hii inaendana na dhamira na azma ya Serikali yetu ya kuwahamasisha na kuwakaribisha watu binafsi, vikundi, kampuni, asasi za kiraia, mashirika ya kimataifa na Serikali za nje kuwekeza hapa nchini ili kukuza uchumi, kupambana na umasikini na kupunguza tatizo la ajira. Hivyo basi, nawapongeza BAKWATA kwa kuitikia wito huo wa Serikali; na nazihimiza Taasisi nyingine za dini nazo ziongeze jitihada za kukuza chumi zao, na kuongeza mapato ili ziweze kumudu kuendesha vyema shughuli zao.

Masuala mengine yaliyozungumzwa kwenye Salamu za Iddi za BAKWATA ni kuhusu malezi bora kwa vijana, masuala ya uhuru, haki, demokrasia, utawala bora na uhuru wa vyombo vya habari. Masuala yote haya ni muhimu. Malezi bora ya vijana ni muhimu sana sio tu katika kuifanya jamii iondokane na vitendo viovu, ikiwemo wizi, ujambazi, rushwa, ubadhirifu wa mali za umma, matumizi ya dawa za kulevya, n.k. Vilevile, yatawafanya vijana washiriki vizuri kwenye shughuli za kimaendeleo na kutoa mchango unaostahiki kwenye familia, jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, nimefurahi BAKWATA mmelizugumzia suala hilo. Kama nilivyosema kwenye Kongamano la Dini pale Dodoma, viongozi wa dini mnaheshimika na kuaminiwa zaidi na wananchi. Hivyo basi, nafasi yenu katika malezi ya vijana na jamii kwa ujumla ni kubwa sana.

Kuhusu suala la haki, uhuru na demokrasia, kama ambavyo nimesema mara nyingi, Serikali itaheshimu na kuimarisha misingi ya haki, uhuru, demokrasia na utawala bora nchini. Hii ni kwa sababu masuala hayo ni muhimu katika kudumisha amani na pia kuchochea ukuaji uchumi.

***Mheshimiwa Mufti na Ndugu Waislamu;***

Sasa naomba nizungumzie suala la ugonjwa wa CORONA, ambalo nalo limo kwenye Salamu zenu za Eid El Fitr mwaka huu. Kwanza, nawashukuru kwa kuwaasa Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa CORONA. Nawashukuru pia kwa kuunga mkono uamuzi wa Serikali kuunda Kamati ya Wataalam ya kushauri namna ya kukabiliana na ugonjwa huu; ingawa mmetoa angalizo kuhusu suala la chanjo. Ninawashukuru sana. Kama nilivyowahi kusema, ugonjwa wa CORONA umeathiri dunia

nzima. Hivyo basi, ili kukabiliana nao hatuna budi kushirikiana na wenzetu duniani.

Hata hivyo, hii haina maana kwamba tutapokea kila kitu tunacholetewa ama kuambiwa. La hasha! Ni lazima na sisi tujiridhishe. Kwa hiyo, hata suala la chanjo nalo tutajiridhisha kabla ya kuamua kutumia au la. Hivyo basi, nawasihi Watanzania kutokuwa na hofu yoyote. Serikali yenu ipo makini sana katika kushughulikia suala hili.

***Mheshimiwa Mufti;***
***Waheshimiwa Masheikh, Ndugu Waislamu;***
***Wageni Waalikwa, na Ndugu Wananchi mnaonisikiliza;***

Leo ni Sikukuu. Ni siku ya kufurahi na kusheherekea. Hivyo basi, sitapenda kuwachosha kwa hotuba ndefu sana. Nihitimishe kwa kurudia kuwashukuru kwa kunialika kwenye Baraza hili la Iddi. Nashukuru pia kwa kuiunga mkono Serikali. Nataka niwahakikishie kuwa, katika kipindi cha Uongozi

wangu nitaendeleza uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati ya Taasisi za Dini na Serikali. Wakati wote milango ya Serikali itakuwa wazi kujadiliana na viongozi wa dini. Na hata nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mufti na Sheikh Mkuu kuwa hata lile suala la tende nalo tutalishughulikia.

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawahimiza waumini wa dini zote nchini kuendelea kuheshimiana na kuvumiliana. Nchi yetu haina dini; lakini Katiba yetu inatoa uhuru wa kila mtu kuamini au kuabudu dini anayoitaka. Kwa hiyo, hakuna sababu ya muumini wa dini moja kugombana ama kubeza dini nyingine. Kufanya hivyo, ni kukaribisha ugomvi kwenye jamii na kuhatarisha amani ya nchi yetu. Hii ndiyo sababu nawasihi sana kuvumiliana na kupendana.

Baada ya kusema hayo narudia kuwatakia Waislamu wote nchini Eid Mubarak. Tuisheherekee kwa amani na furaha; bila ya kufanya vitendo vya kumchukiza Mwenyezi Mungu.

***Eid Mubarak!***

***Assalam Aleykum!***

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

**"Asanteni Sana kwa kunisikiliza"**